JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

## TAARIFA YA HALI MBAYA YA HEWA KWA MWEZI JANUARI NA FEBRUARI, 2026

### 1.0 UTANGULIZI

Katika kipindi cha mwezi Januari 2026, baadhi ya maeneo nchini yalipata mvua hususan maeneo ya ukanda wa pwani, Ziwa Victoria Pamoja na magharibi mwa nchi. Aidha, vipindi vichache vya mvua kubwa katika mwezi Januari.

Katika kipindi cha mwezi Februari, 2026, vipindi vya mvua ya wastani hadi mvua kubwa vilijitokeza katika maeneo mengi nchini, ikijumuisha maeneo ya ukanda wa pwani, ziwa Viktoria pamoja na magharibi mwa nchi. Aidha, ongezeko la mvua lilijitokeza wiki ya tatu na ya nne ya mwezi. Vipindi vya mvua kubwa vilijitokeza katika maeneo ya kusini mwa nchi, nyanda za juu kusini magharibi, nyanda za juu kaskazini mashariki na pwani ya kusini.

Kwa ujumla, hali ya hewa iliyojitokeza pamoja na athari zake imeendana na taarifa ya mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba 2025 – Aprili 2026).


### 1.1 Mvua kubwa kwa mwezi Januari, 2026

Katika kipindi cha mwezi Januari, vipindi vya mvua vilijitokeza katika baadhi ya maeneo. Aidha, vipindi vichache vya mvua kubwa vilijitokeza katika kipindi hiki. Kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 84.0 ndani ya saa 24 kiliripotiwa katika kituo cha Tabora ikifuatiwa na milimita 63.0 katika kituo cha Tumbi (mkoa wa Tabora) mnamo tarehe 28 Januari, 2026. Vituo vilivyoripoti vipindi vya mvua kubwa vya milimita 50 au zaidi ni kama vinavyoonekana kwenye Kielelezo namba 1.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu “N”, Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*728G _ 02/2026*




**Kielelezo 1**: Viwango vya mvua kubwa kwa mwezi Januari 2026

**1.2 Hali joto kwa mwezi Januari, 2026**

Katika kipindi cha mwezi Januari, 2026 viwango vya joto la juu vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, hususan ukanda wa pwani na maeneo machache ya nyanda za juu kaskazini mashariki.
Kwa nyakati za mchana, viwango vya juu vya joto viliongezeka kidogo katika baadhi ya maeneo nchini. Mkoa wa Kilimanjaro ulikuwa na hali ya joto zaidi, ambapo kwa siku 8, viwango vya juu vya joto vilikuwa nyuzi joto 35°C au zaidi. Kiwango cha juu zaidi cha joto cha nyuzi joto 37.5°C kiliripoti mnamo tarehe 21 Januari, 2026 katika kituo cha Mlingano (Mkoa wa Tanga).

**Jedwali 1**. Idadi ya siku ambazo viwango vikubwa vya joto la juu vilijitokeza kwa mwezi Januari, 2026


| Kanda | Kituo | Idadi ya siku (≥ 35°C) | Kiwango cha joto la juu zaidi kurekodiwa ($^0$C) |
|---|---|---|---|
| Nyanda za juu kaskazini mashariki | Kilimanjaro | 8 | 36.5 °C |
| | Moshi | 6 | 36.2 °C |
| Pwani ya Kaskazini | Mlingano | 2 | 37.5 °C |
| | Ilonga | 2 | 35.7 °C |
| | Morogoro | 2 | 35.6 °C |

### 1.3 Upepo Mkali kwa mwezi Januari, 2026

Katika mwezi Januari 2026, upepo wa kawaida uitawala katika maeneo mengi. Hakukua na vipindi vya upepo mkali unaozidi kilomita 40 kwa saa.

### 1.4 Mvua kubwa kwa mwezi Februari, 2026

Katika kipindi cha mwezi Februari, 2026 vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, huku vipindi vifupi vya mvua kubwa viliripotiwa katika baadhi ya vituo. Kiwango cha juu zaidi vya mvua vya milimita 105.1 mnamo tarehe 21 Februari katika kituo cha Same (Mkoa wa Kilimanjaro), ikifuatiwa na milimita 91.9 na 86.4 mnamo tarehe 26 Februari 2026 vilipimwa katika katika vituo vya hali ya hewa vya Handeni (Tanga) na Kilimanjaro mtawalia. Vituo vingine vilivyoripoti vipindi vya mvua kubwa vya milimita 50 au zaidi ni kama vinavyoonekana kwenye Kielelezo 2.




**Kielelezo 2:** Viwango vya mvua kubwa kwa mwezi Februari, 2026

Taarifa za vyombo vya habari zilithibitisha kuwepo kwa athari mbalimbali zilizotokana na mvua zilizonyesha katika kipindi cha mwezi husika. Mnamo tarehe 25 Februari, mvua kubwa iliyoambatana na upepo mkali ilinyesha kwa saa kadhaa katika Jiji la Arusha, na kusababisha mafuriko katika maeneo mbalimbali. Hali hiyo iliathiri kwa kiasi kikubwa shughuli za usafiri na kiuchumi. (*Chanzo: Arusha Zone*).



**Kielelezo 3:** Barabara ikiwa imefurika maji na kupitika kwa shida baada ya mvua kubwa kunyesha jijini Arusha. *(Chanzo: Arusha Zone Media)*

**1.5 Hali joto kwa mwezi Februari, 2026**

Katika kipindi cha mwezi Februari, 2026 hali ya joto hadi joto kali iliendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchini. Kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 37.8 °C kilirikodiwa katika kituo cha uwanja wa ndege wa kimataifa wa Kilimanjaro mnamo tarehe 11 Februari, 2026. Mlingano iliendelea kuwa na siku nyingi zenye joto zaidi ukilinganisha na maeneo mingine amabapo kwa siku 9 viwango vya juu vya joto vilifikia au kuzidi nyuzi joto 35 °C. Vituo vingine vilivyoripoti viwango vya joto vya nyuzi joto 35 au zaidi vimeainishwa kwenye jedwali namba 2.

**Jedwali 2**. Idadi ya siku ambazo viwango vikubwa vya joto la juu vilijitokeza kwa mwezi Februari, 2026

| Kanda | Kituo | Idadi ya Siku (≥ 35°C) | Kiwango cha Joto la juu zaidi Kurekodiwa ($^0$C) |
|---|---|---|---|
| Nyanda za juu kaskazini mashariki | Kilimanjaro | 6 | 37.8 °C |
| | Moshi | 6 | 36.2 °C |
| Pwani ya Kaskazini | Mlingano | 9 | 35.7 °C |
| | Zanzibar | 1 | 35.7 °C |
| | Kibaha | 1 | 35.8 °C |
| | Dar es salaam | 1 | 35.0 °C |

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu “N”, Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

### 1.6 Upepo Mkali kwa mwezi Februari, 2026

Katika kipindi cha mwezi Februari, vipindi vya upepo mkali, wenye kasi ya kilomita 40 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo, ikiwemo maeneo ya ukanda wa pwani, Ziwa Victoria na nyanda za juu kaskazini mashariki, hususani mkoa wa Kilimanjaro.

*Matukio haya ya hali mbaya ya hewa yanaonesha ongezeko la changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na umuhimu wa kutekeleza mikakati thabiti ya kukabiliana mabadiliko hayo ili kulinda jamii na mazingira*.

*Imetolewa: tarehe 24 Machi, 2026*
**Na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**